**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI SOLYA – HALMASHAURI YA WILAYA MANYONI

**Tarehe......................**

**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI SOLYA**

S.L.P 11,
MANYONI,
SINGIDA.
Tarehe…………

Mkuu wa Shule: ZAINABU ISIMA MTINDA
Simu: **0716723373/0755278326/0787723373**
Makamu mkuu wa shule: 0762484746/0769609911
Matron/malezi: **0758017016/**

NDG. MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI: …………………………………

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA **SOLYA**, HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI MKOA WA SINGIDA

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya wasichana ya mkoa wa Singida; SOLYA SEKONDARI iliyopo Wilaya ya Manyoni katika Mkoa wa Singida mwaka……………katika Tahasusi ya PCB/PCM/PMC/PGM.
**HONGERA NA KARIBU SANA SOLYA SEKONDARI.**
2. Shule iko kilometa 20 kutoka Manyoni mjini.
Kama utatokea uelekeo wa Manyoni Mjini, ni umbali wa kilomita 20, mara tu baada ya kumaliza Mlima mdogo wa Muhalala utakuwa umekaribia kituo cha mabasi Solya; ukishuka hapo utaelekezwa shule ilipo na kama utapanda boda boda nauli ni shilingi elfu moja (1000) au unaweza kuomba msaada kwa mwenye basi akushushie kwenye kibao cha shule; utakuwa umefika shuleni.
Shule ipo barabarani; Barabara kuu ya Dodoma, baada ya ‘’rezevu’’ ya Barabara yanafuatia Majengo ya Shule;
3. Kama unatokea uelekeo wa Dodoma; ukimaliza mlima Saranda utakuwa umekaribia na baada ya Sukamahela kituo kinachofuata ni SOLYA. Utaomba ushushwe kwenye kibao cha Shule ama usiposhushwa basi utashukia stand ya Solya. Maelezo namba 2 yanajitosheleza.

Muhula wa masomo utaanza…………………...
Aidha una muda mrefu wa kumuandaa mtoto hakuna sababu ya kuchelewa kuripoti Shule! Ninasisitiza mwanafunzi afike shuleni mapema bila kuchelewa, muda wa

kuripoti ni kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na moja na nusu jioni. Kama kuna dharura tumia namba za shule kuutarifu uongozi wa Shule.

### 4. MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA:

4:1. Kadi ya NIDA kama anayo aje nayo tafadhali.

4:4: SARE ZA SHULE

a) Sare ya shule ni sketi mbili (2) za DRAFTI (MAROON, DARK BLUE NA NYEUPE) Mshono wa Rinda box (V shape) kwa mbele; iwe ndefu kawaida ifunike magoti; isipuungue urefu wa sentimita 15 kutoka kwenye magoti; kwa wanafunzi wa dini ya kiislamu sketi iwe ndefu mpaka chini. Tai ndefu yenye kufanana na sketi (kwa wanafunzi wasiovaa hijabu)
b) Mashati mawili ya mikono mirefu, rangi ya bluu Bahari iliyopauka (light blue)
c) Shati moja la mikono mifupi rangi ya bluu Bahari iliyopauka (light blue)
d) Kizibao kimoja; rangi ya blue iliyokolea chenye shingo ya “V” na ufito wa uzi mweupe shingoni na chini.
e) Wanafunzi wanaovaa hijabu (kijuba) iwe blue bahari iliyopauka (ifanane na rangi ya shati) na iwe ndefu kufika usawa wa nyonga, zingatia: hijabu zote ziwe za kitambaa cha blue bahari iliyopauka rangi ya kufanana na shati. (hijabu isiwe ya kitambaa cha mpira tafadhali)
f) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, Jozi mbili (2)
g) Sare ya michezo ni bukta na T-shirt rangi ya blue iliyokolea, raba rangi nyeupe (jozi moja) na traki suti nzito rangi ya kijivu (jozi moja)
h) Soksi ndefu nyeupe (stoking) kuanzia jozi mbili; nasisitiza ziwe ndefu
i) Sweta la **dark blue** yenye shepu ya V mbele – shingoni
j) Nguo za kushindia (shamba dress) sketi nyeusi moja au mbili marinda ya kupanga (mbele marinda nane au saba na nyuma vivyo hivyo) jumla marinda 16 au 14, iwe ndefu
k) Tisheti mbili za kushindia rangi ya Kijivu iliyokolea
l) Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa isipokuwa aje na kanga/vitenge jozi moja tu, atatumia wakati wa kuoga.
m) mwanafunzi anaweza kununua pull neck (sweta la kaba shingo) NYEUPE ya kuvalia ndani ya shati la shule nyakati za baridi – SIO LAZIMA

NOTE: Kwa mzazi anayetaka anaweza kupata baadhi ya mahitaji shuleni (NI HIYARI YA MZAZI) kwa bei zifuatazo: sketi ya draft moja shilingi 26,000/= sketi nyeusi moja 20,000/= shati la mikono mirefu moja shilingi 14,000/= shati la mikono mifupi shilingi 11,000, kizibao shilingi 15,000/= tisheti ya kijivu yenye nembo ya shule 13,000/= tai shilingi 3000/= godoro 55,000/=

**2:2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:**

i. Madaftari makubwa (counter book quire 4 nane (8) madaftari nane na madaftari ya msomi madogo 8 kwa ajili ya majaribio ya ndani.
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa ajili ya shughuli za Kitaaluma.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Dissection Kit **ILIYOKAMILIKA (kwa wanafunzi wenye somo la biology)**
v. Scientific Calculator, na stop watch, mathematical set
vi. Godoro la sponji futi 2.5 inch 4 na mto wa kulalia
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki na foronya zake, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*nyeupe ya pembe nne).*
viii. Nguo za ndani za kutosha na taulo za kike za kutosha
ix. Sanduku gumu la chuma (tranka) kwa ajili ya kuhufadhia vifaa vyake
x. File moja – kwa ajili ya kuhifadhia mitihani na majaribio yake
xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xii. Ndoo 2 , moja ya lita 20 na ya pili ndoo ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na dumu la lita tano la kuhifadhia maji ya kunywa

VIFAA VYA USAFI

I. Ufagio mmoja mlaini (soft broom) na chelewa kwa kila mwanafunzi.
II. Dawa ya chooni aina ya ARO kwa wanafunzi wote.
III. Jembe moja lenye mpini kwa kila mwanafunzi
IV. Reki moja kwa wanafunzi wa PCM
V. Kwanja moja kwa mwanafunzi wa PCB
VI. Panga moja kwa wanafunzi wa PGM
VII. Ufagio wa kukaushiamaji (squizer) PMC

**VIII. Kila mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA**; kama hana bima ya afya aje na shilingi **50,400/= kwa ajili ya Bima – (Pesa ya Bima isiwekwe Bank)**

**2:3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha zote kwenye jedwali hapo juu zilipwe kwenye akaunti ya shule **0150865986200 – Solya Secondary school – CRDB –** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Bank pay in slip) aje nayo anaporipoti shule

1. **Sheria na Kanuni**

   Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara yenye dhamana ya elimu ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni:

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote kulingana na muda husika
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Huruhusiwi kwenda kwenye nyumba za Watumishi
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa "MALAPA" kwenye ukumbi wa Chakula na sehemu yeyote ile anapokuwa nje ya sare za darasani
**xiii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.**

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule mara inapothibitishwa kuwa kuna ulazima huo.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi wa mali za shule, mali za watumishi za jamii na mali za wanafunzi wengine;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuolewa;

x. Kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

KARIBU SANA SOLYA SEKONDARI!

**"WE ARE LEARNING, LEADING AND ILLUMINATE"**

2. **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOTAJWA MWANZO WA MAELEKEZO HAYA**

3. **Tafadhali fomu/vipimo vya Hospitali vya kuthibitisha afya ya Mtoto ijazwe/vipimwe kikamilifu kuthibitisha afya ya Mtoto. Fomu ya Hospitalini imeambatanishwa**

......................................

**ZAINABU ISIMA MTINDA**
**MKUU WA SHULE**

SOLYA GIRLS SECONDARY SCHOOL
HEAD OF SCHOOL
P. O. Box 11
MANYONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SOLYA**

**FOMU YA MAKUBALIANO.**

**Habari za mwanafunzi:**

1) Jina kamili ………………………………………………………………
2) Tareh ya kuzaliwa ………………………wilaya……………………..
3) Dini………………………..dhehebu…………………………………
4) Mahali atakapokuwa anaenda likizo………………………………….
5) Ndugu watakaoruhusiwa kuja kusalimia (Jumamosi ya mwisho wa mwezi)
   Jina ……………………………………………..uhusiano…………
   Jina ……………………………………………...uhusiano…………

**Tamko la Kukubali:**

**Mimi ……………………………………………….(majina matatu ya mwanafunzi)** nimesoma maelekezo ya kujiunga na shule ya wasichana ya SOLYA Sekondari. Nakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni Pamoja na kutii sheria za shule nitakapokuwa Shuleni. Nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidi na kuchapa kazi za mikono kwa bidii, **kutunza mazingira**, kushiriki kikamilifu ratiba yote ya shule ili kutimiza malengo yangu, malengo ya shule na Taifa kwa ujumla**. NA NINAAHIDI KUWA MWANAFUNZI MWEMA, MTIIFU MWENYE NIDHAMU YA HALI YA JUU NIKIONGOZWA NA MOTTO WA SHULE.**

SAINI…………………………………..TAREHE…………………….

Habari na uthibitisho wa mzaazi/mlezi

i. Jina kamili la Mzazi/Mlezi……………………………………...
ii. Uhusiano uliopo na mwanafunzi………………
iii. Kazi yake………………………………………..
iv. Anwani ya kazini……………………..………
v. Namba ya simu…………………….……………
vi. Anwani ya nyumbani…………….……………

Uthibisho wa mzazi/mlezi:

Nimejiridhisha kuwa maelekezo na maagizo yameeleweka na mtoto wangu atafuata sheria na taratibu zote za shule na nitatoa ushirikiano wa hali ya juu dhidi ya malezi ya mtoto

Saini………………………………tarehe…………………………………………..

**MANYONI DISTRICT COUNCIL**
**SOLYA SECONDARY SCHOOL**

SOLYA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 11
**MANYONI**
Date ………………………

To the Medical Officer
……………………………………………………..
……………………………………………………..
……………………………………………………..
Dear Sir/ Madam

RE: **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine Miss……………………………………………………… as to her fitness to join our school

Yours Sincerely,
HEAD OF CHOOL

…………………………………………
ZAINABU ISIMA MTINDA
MKUU WA SHULE

**TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER**

**DECLERATION**

I have examined Miss ……………………………………… and certify that she is

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

**…………………………………………** **…………………………………………..**

**Name of Medical Officer** **Signature of Medical Officer**

**Designation ……………………… Official Stamp ………………………**